

**HOTUBA YA MKUU WA WILAYA YA WANGING'OMBE MHE. JOHN
KANONI KATIKA UZINDUZI WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA
MASAULWA UNAYOFADHILIWA NA TASAF KUPITIA MPANGO WA
KUPUNGUZA UMASKINI AWAMU YA NNE (TPRP IV) MAARUFU KAMA
OPEC IV, KATIKA KIJJI CHA MASAULWA
TAREHE 25/05/2022**

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Wakuu wa Idara na vitengo
Mheshimiwa Diwani
Afisa Mtendaji wa Kata
Mwenyekiti wa Kijiji
Afisa Mtendaji wa Kijiji
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

**Ndugu wananchi, NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA:**

Awali ya yote, nichukue nafasi hii kushukuru Uongozi wa TASAF kwa kunipa fursa hii ya kujumuika nanyi na kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa Mradi huu wa Ujenzi wa Zahanati katika kijiji cha Masaulwa unaotekelezwa kupitia fedha za Kupunguza Umaskini – OPEC awamu ya nne mwaka wa kwanza.

Ndugu wananchi, Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF kilizinduliwa tarehe 17 Februari 2020 Jijini Dar es Salaam, tulianza na zoezi la kuahakiki kaya maskini katika vijiji vilivyo kwenye mpango, na kufuatiwa na zoezi la uandikishaji wa kaya maskini kwa vijiji ambavyo havikuwepo katika mpango, ni jambo la kuishukuru Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Jemedari wetu, mama yetu, Mhe. Samia Suluhu Hassani kwa kuhakikisha Vijiji vyote sasa vipo katika mpango. Miradi ya TPRP IV inatekelezwa katika Mikoa mitano tu ya Tanzania, ambayo ni Arusha, Mwanza, Geita, Simiyu na Mkoa wetu wa Njombe.

Ndugu wananchi; Katika awamu hii, Wilaya imefanikiwa kuibua miradi 10 ya ujenzi katika sekta ya Elimu, maji na Afya ambapo Jumla ya Tsh. **758,694,348.45** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi tisa kati

ya 10 iliyoombwa; miradi mitano hiyo ipo katika kijiji cha Utiga, mradi mmoja kijiji cha Mapogolo, Usuka mradi mmoja ,Banawanu mradi mmoja na mradi mmoja wa ujenzi wa zahanati, matundu manne ya vyoo na kichomea taka upo katika kijiji hiki cha Masaulwa; mradi wenye thamani ya **Tsh 101,452,733.62**, hongereni sana. Niwasihi msiitumie vibaya bahati mliyoipata zaidi niwapongeze na natumia fursa hii kusisitiza yafuatayo:-

Jambo la kwanza, mnapaswa kusimamia utekelezaji wa mradi siku hadi siku kwa uaminifu na uadilifu mkishirikiana na wataalam wa ngazi ya halmashauri ili mradi huu ukamilike kwa wakati na ubora wa hali ya juu ukitoa thamani halisi ya fedha iliyotumika.

Aidha;

(a) Manunuzi ya vifaa na huduma kwa ajili ya mradi yafanyike kwa uaminifu na kwa kuzingatia Miongozo, kanuni na taratibu mlizoelekezwa kupitia mafunzo mliopewa

(b) Kuhifadhi vifaa, vitabu vya hesabu na kumbukumbu za stoo sehemu salama na kwa umakini mkubwa.

(c) Kuhakikisha kuwa michango ya jamii inapatikana kama makubaliano yalivyo katika Mkataba wa maombi ya fedha toka TASAF.

(d) Utekelezaji wa mpango wa hifadhi ya mazingira unazingatiwa kwa kuhakikisha uwepo vyoo vya muda mfupi pamoja na sanduku la huduma ya kwanza. Lakini mara tu baada ya kukamilika kwa mradi miti ipandwe kuzunguka eneo la mradi pamoja na maua.

Ndugu wananchi jambo la pili, jamii inapaswa kuchangia na kushiriki kikamilifu kwa hali na mali, ambapo kutakuwa na michango ya fedha taslimu, lakini pia kuchangia nguvu kazi kwa kushiriki katika shughuli zifuatazo:

Kuteka maji; Kubeba matofali wakati wa ujenzi; Kukusanya na kusomba mchanga kupeleka kwenye eneo la mradi; Kusomba mawe kupeleka kwenye eneo la mradi; Kufyatua matofali ya kuchoma; Kufyatua matofali ya saruji; Kutoa usafiri na kusafi risha vifaa vya ujenzi; Kushusha vifaa kutoka kwenye magari ya mizigo; Kusafisha eneo la ujenzi kabla ya kuanza ujenzi; Kuchimba mtaro wa msingi; Kuchimba mashimo ya vyoo; Kubeba vifaa vya ujenzi kutoka stoo kwenda eneo la ujenzi; Kutoa ardhi kwa ajili ya mradi;

Muda utakaotumika kwa mikutano inayohusu mradi; Kuchimba mitaro ya mabomba ya maji; Usimamizi wa mradi unaofanywa na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Jamii; Kufanya kazi za kuwasaidia mafundi.

Shughuli zote hizi zinaweza kupewa thamani ya bei ya soko kwa kutumia viwango vya malipo ya kazi hizo vinavyotumika kwa wakati husika.

Ndugu wananchi; Uhamasishaji wa michango ya jamii si kazi ya mtu mmoja, ambapo kila mmoja ahamasike yeye binafsi na amhamasishe jirani yake, aidha utaratibu utafanyika kwa Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Jamii (CMC) kuwasilisha mahitaji kwa Halmashauri ya Kijiji na Uongozi wa Kijiji utatengeneza utaratibu wa michango kwa vitongoji, kaya ama watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Hivyo tuwe tayari wakati wote kujitoa kwa hali na mali ili kukamilisha Mradi huu ndani ya muda uliopangwa.

Mwisho

Ndugu wananchi; hatutarajii Mradi huu ukaifanya Wilaya ya Wanging'ombe kupata dosari, nasisitiza tena Wataalam, viongozi na jamii kwa ujumla mvae silaha zote za utawala bora pamoja na uwazi, uadilifu, uzalendo, weledi, na uaminifu katika kutekeleza, kusimamia na kukamilisha Mradi huu; mtarajie kupokea ugeni wakati wowote, hivyo muwe tayari kwa kuweka nyaraka zenu vyema na taarifa za mradi zinazoeleweka. Aidha niwapongeze na kuwatakia utekelezaji mwema wa majukumu mliopewa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAZI IENDELEE